

»Kulisha panya wakatanyasi«

Mkatanyasi ni panya mpya wa msituni anayefugwa nyumbani. Waafrika wengi hufurahiya kula nyama yake. Kufuga mkatanyasi ni shughuli nzuri ambayo huingiza mapato, kwani hauhitaji fedha nyingi kuanzisha mradi huo.

Ili kufanikiwa na ufugaji huu, andaa makazi mazuri wa wanyama, wachunguze kwa makini, na wape lishe ya usawa. Chakula chao kimsingi ni lishe ambacho ni pamoja na nyasi za kudumu kama vile *panicum*, *pennisetum* ambazo zinaweza kuvunwa kutoka porini au kulimwa. Majani ya mitende, nafaka, mashina na njugu.

Nyasi na matunda

Lishe linaweza kuongezwa na matunda ambayo hayajaiva kama vile papai na maembe. Matunda yaliyoiva yaepukwe kwa sababu husababisha kuhara na uvimbe. Miwa, mizizi ya nyasi, mihogo na viazi vikuu vilivyokatwa katika vipande vidogo pia vinaweza kuongezwa. Uangalifu unafaa kudumishwa wakati wa kuwalisha wanyama mihogo, kwani mihogo zingine zina uchungu na sumu. Zizi lazima zisafishwe. Walishe wakatanyasi kiwango cha kutosha cha lishe kila asubuhi, mchana na jioni. Mizizi na miwa inafaa kupunguzwa kwani inathiri ukuaji na meno ya wakatanyasi.

Lishe la mchanganyiko

Malishe hutayarishwa nyumbani kwa kuchanganya mahindi, mafuta, wishwa ya ngano na chumvi. Malishe haya huongezwa pamoja na vipande vidogo vya mizizi, matunda ambayo hayajaiva, na maji kwani ni rahisi kuliwa kwa mnyama.

Malishe yaliyochanganywa husaidia wakatanyasi kuzaa watoto wenye nguvu, ukuaji bora na afya. Malishe yaliyolainishwa kuwa unga husababisha magonjwa ya kupumua.

Kuvuna Lishe

Uvunaji hufanyika mchana kwa sababu umande wa asubuhi hubeba vimelea. Lishe lililovunwa huhifadhiwa kwa muda kadha kabla ya kulishwa wakatanyasi. Hii husaidia kuzuia magonjwa kama vile kuhara unaosababishwa na vimele katika lishe iliye unyevu.

Kutambua lishe lililokomaa

Lishe ambalo lina kiwango cha fumuele cha kutosha huvunwa. Panicum iliyokomaa ina maua, shina lake lina tundu ndani likikatwa. Pennisetum, huwa tayari wakati shina huanzu kuonekana.